# Hadithi 24

## KATIKA ALAMA KUBWA ZA KIAMA

Kutoka kwa Abu Hurayrah Mwenyezi Mungu awe radhi naye amesimulia kutoka kwa Mtume Rehma na Amani zimshukie amesema:

"Harakisheni kutenda matendo mema kabla ya kudhihiri mambo sita:

1. Kuonekana Masihi Dajjal
2. Kudhihiri Moshi,
3. Kutokea Mnyama katika dunia,
4. Jua Kuchomoza kutoka magharibi.
5. Amri ya watu wote,
6. Kifo cha mmoja wenu[1].

1 Muslim (2947).

### Ayah

Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

- *﴿Na yakimbilieni maghfira ya Mola wenu Mlezi, na Pepo ambayo upana wake ni mbingu na ardhi, iliyo wekwa tayari kwa wachamngu﴾ [Al Imran: 133].*
- *﴿Siku zitakapo fika baadhi ya Ishara za Mola wako Mlezi, kuamini wakati huo hakutomfaa mtu chochote, ikiwa hakuwa ameamini kabla yake, au amefanya kheri katika Imani yake. Sema ewe Muhammad: Ngojeni, nasi pia tunangoja﴾ [Al-An'am: 158].*
- *﴿Na itapo waangukia kauli juu yao, tutawatolea mnyama katika ardhi atakaye wasemeza, ya kuwa watu walikuwa hawana yakini na Ishara zetu﴾ [An-Naml: 82].*
- *﴿Basi ingoje siku ambayo mbingu zitakapo leta moshi ulio dhaahiri (10) Utakao wafunika watu: Hii ni adhabu chungu (11) Mola wetu Mlezi! Tuondolee adhabu hii. Hakika tutaamini (12)﴾ [Ad Dukhan: 10-12]*

### Msimulizi

Ni: Abu Hurayrah, na jina lake – kwa Kauli sahihi – ni: Abd al-Rahman bin Sakhr al-Dawsi, Al Azdi, al-Yamani, alisilimu katika mwaka wa vita vya Khaybar, Basi akashikamana na Mtume, Rehma na Amani zimshukie, na alikuwa na shauku ya kujifunza na kuhifadhi Hadith. Ndipo Mtume amani iwe juu yake, akamuombea Dua ili asisahau;
Na ndiye aliyepokea hadithi nyingi kati ya Maswahaba. Alifariki Madina katika mwaka wa (58 H)[1].

### Muhtasari

Mtume Rehma na Amani zimshukie ametaja baadhi ya alama za Kiyama zitakazokuja kwa ghafla, na Mtume Rehma na Amani zimshukie anawaamrisha watu wake kuharakisha kutenda matendo ya kheri kabla ya kuonekana dalili hizo.

1 Unaweza kurejea historia yake katika kitabu: "Maarifaat al-Sahaba" cha Abu Nu'aym (4/1846), ""Al istie`ab Fi Maarifat Al'as-habi"" cha Ibn Abd al-Bar (4/1770), "Asad al-Ghaba" cha Ibn Al-Atheer (3/357), ""Al'iisabat Fi Tamayuz Alswahabati"" cha Ibn Hajar Al-Asqalani (4/267).

# Ufahamu

1 Mtume Rehma na Amani zimshukie Ametuamrisha tuharakishe kutenda mambo ya kheri kabla ya kudhihiri mambo sita yanayomshughulisha mtu na kumzuia kufanya mambo mema, ni kabla ya kuchomoza jua kutoka magharibi, ambapo likichomoza kutoka upande wa magharibi haitakubaliwa ibada yoyote wala toba.

2 Jambo la kwanza kati ya hayo ni kutokezea kwa Mpinga Kristo – Masihi ad Dajjal-. Na yeye ndiye mtihani mkubwa zaidi duniani, lakini yeye ni binadamu mkubwa, macho yake yamefutiwa, na neno "kafiri." limeandikwa kwenye paji la uso wake, atadhihiri zama za mwisho na kudai kuwa yeye ndiye Mungu - Ametakasika mno Mwenyezi Mungu Mtukufu juu ya hayo madai ya batili, Na Mwenyezi Mungu akamuunga mkono kwa nguvu zisizo za kawaida, ili kuwazidishia watu majaribu, Dajjal ataamrisha mvua inyeshe na mvua itanyesha, na kisha ardhi itamea na kustawi vizuri.Na ataamrisha ardhi itowe hazina zake na zitatoka na kumfuata, na atampasua mtu sehemu mbili, kisha atasimama kati ya sehemu zake mbili na kumwita, naye ataitika na kunyanyuka akiwa hai, na habari zake nyingine zinazojulikana, ataendelea kuwa hivyo mpaka Masihi Isa bin Maryam, amani iwe juu yake, atakaposhuka na kuliongoza jeshi la Waislamu na kumuua.

Alianza kwa kumtaja Mpinga Kristo -masihi Ad Dajjali- ambapo ishara za kiyama zitapishana kwa kuja kwake, na hivyo dalili za kiyama zitakuja mfululizo, ishara baada ya ishara, mpaka kiyama kusimama. Amesema Mtume Rehma na Amani zimshukie: "dalili za kiyama ni kama shanga zilizounganishwa na waya, hivyo utakapokatwa waya hufuatana baadhi kwa baadhi"(1).

3 Ya pili: kuonekana kwa moshi, nayo ni miongoni mwa alama za kiyama, utakaa katika ardhi siku arobaini, utajaa mbinguni na ardhini. Ama Muumini atapigwa nayo kama baridi tu, lakini makafiri na mafisadi Moshi huo utawaingia puani mwao na kutoboa masikio yao, na utapunguza pumzi yao Siku ya Kiyama(2), Moshi huo ni athari za Jahannamu. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: ""Basi ingoje siku ambayo mbingu zitakapo leta moshi ulio dhaahiri (10) Utakao wafunika watu: Hii ni adhabu chungu (11) Mola wetu Mlezi! Tuondolee adhabu hii. Hakika tutaamini (12)" [Ad Dukhan: 10-12]

4 Ya tatu: Mnyama atakaetokea zama za mwisho atakuwa akiwasemesha watu, Mwenyezi Mungu amesema: "Na itakapowathibitikia kauli juu yao, tutawatolea mnyama katika ardhi atakaye wasemeza, ya kuwa watu walikuwa hawana na yakini na Ishara zetu" [An-Naml:

1 Al-Hakim katika "Al-Mustadrak" (8639).

2 Tazama: Al-Jami` Al-Ahkam Al-Qur'an cha Al-Qurtubi (16/130).

82]. Qur'ani wala Hadith za Mtume (s.a.w.w.) hazikuweka wazi umbile la mnyama huyu, hivyo ni Mwenyezi Mungu pekee ndiye anajua zaidi kuhusu hilo.

Ishara ya Kutokea mnyama ni mara tu baada ya jua kuchomoza kutoka magharibi. Kwa sababu Mtume Rehma na Amani zimshukie amesema: "Dalili ya kwanza kutokea, ni jua kuchomoza upande wa magharibi tofauti na kawaida yake, na Mnyama kuwadhirikia watu nyakati za asubuhi, itakapotokea moja kati ya hizo mbili, basi nyengine itafuata baada yake punde tu"[1].

5 Na ya nne: kuchomoza kwa jua kutoka magharibi - kama halikuzoeleka linapochomoza mashariki -;Katika Hadith sahihi Mtume Rehma na Amani zimshukie anasema: "Jua linapotua, huenda kusujudu chini ya Arshi -kiti cha enzi- Basi linaomba ruhusa, na linapewa ruhusa, na linakuwa karibu na kusujudu, lakini halitakubaliwa, na litaomba ruhusa, na halitaruhusiwa, bali litaambiwa: Rudi ulikotoka na uchomoze kutoka upande wa magharibi"[2].

6 Ya tano: ufufuo, Mtume aliuita hivyo kwa sababu unawakumba watu wote kwa mauti na haumwachi yeyote[3], hakika mwanadamu kiyama kitakaposimama, atajutia kila alichopuuza na kufupisha; Wakati huo, Muumini atatamani lau angeongeza utiifu. Na kafiri atatamani kwamba wakati umrudie ili atubu kutokana na hali atakayo kuwa nayo siku hiyo.

7 Ya sita: ni mauti; Na Mtume akaiita khweisah ya mmoja wenu kwa sababu inamhusu mwanadamu na sio viumbe wengine, kinyume na ufufuo ambapo aliuita kuwa ni amri ya watu wote.

Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwaamrisha waja wake watubu na watende mema kabla ya kufa kama alivyo sema: Enyi mlio amini! Yasikusahaulisheni mali yenu, wala watoto wenu, kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Na wenye kufanya hayo ndio waliopata hasara (9) Na toeni katika tulicho kupeni kabla hayajamfikia mmoja wenu mauti, tena hapo akasema: Mola wangu Mlezi! nicheleweshe muda kidogo nipate kutoa sadaka, na niwe katika watu wema (10) Wala Mwenyezi Mungu hataichelewesha nafsi yoyote inapofika ajali yake; na Mwenyezi Mungu anazo khabari za mnayo yatenda" [Al Munafiqun: 9-11].

1 Muslim (2941).

2 Al-Bukhari (3199) na Muslim (159).

3 "Mwisho katika Gharib Al-Hadiyth na Al-Athar" cha Ibn Al-Athiir (3/302).

# Mafunzo

1. Tukumbuke shauku ya Mtume Rehema na Amani zimshukie, na tukumbuke huruma zake kwa ummah wake, kwa kuuelekeza juu ya nyakati ambazo baada yake imani haitawafaa, ili wafanye haraka katika mambo ya wema kabla ya nyakati hizo, Hivyo Mja anapaswa kuwa na shauku zaidi ya kufuata amri hiyo ya unabii, na kuharakia matendo ya haki kabla ya dalili hizi kuonekana.

2. Maswahaba wamezipokea Hadiyth zile ambazo akili ya mwanadamu inaweza kutatanishwa, wakazikubali na kuzisimulia, kwa sababu ya ukamilifu wa dini yao na akili zao, bila shaka walijua ukweli wa Mtume, na ukamilifu wa elimu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, basi mwenye akili timamu anazikubali kwa kunyenyekea, na wala haogopi kuzisomesha.

3. Muumini afanye hima kutubia na kuomba msamaha na aharakishe kutenda mema kabla ya muda kufika. Mwenyezi Mungu ni mwingi wa kusamehe, hunyoosha mkono wake wakati wa usiku ili watubie wakosefu wa mchana, na hunyoosha mkono wake mchana ili watubie wakosefu wa usiku, na husamehe madhambi yote pasina kujali.

4. Mtume Rehema na Amani zimshukie mara kwa mara aliuonya umma wake dhidi ya Mpinga Kristo- Masihi Ad Dajjal- kutokana na hatari yake kubwa na vitimbi vyake.

5. Ni juu ya Walinganiaji na Wanachuoni kutilia umuhimu mitihani inayoweza kuwapata Waislamu, na kuwaeleza fitina zitakazowakfika, na kuwakumbusha hukumu ya Mwenyezi Mungu katika matukio halisia ya hivi karibuni, wajitahidi khutba zao, habari na maandishi yao yasiwe mbali sana na hali halisi ya jamii wanayo ishi.



**Amesema mshairi:**

*Ewe nafsi, kuondoka kumefika = na hotuba tukufu zitakufunika.*

*Kwa hivyo zinduka ewe nafsi, = isikuchezee shere mipango na mikakati mirefu ya kidunia.*

*Usipozinduka fahamu kuwa utaishi katika nyumba mtu atamsahau rafiki yake kipenzi.*

*Utatupiwa juu yako mzigo mzito = katika udongo na hutaweza kuunyanyua.*

*Tulipangiwa mikakati ya kuondoka duniani, hatobaki mtukufu wala mtu dhalili.*



